# HOTUBA YA MKUU WA CHUO CHA ARDHI MOROGORO BW. HURUMA L. P. LUGALLA ILIYOTOLEWA KWENYE MAHAFALI YA AROBAINI (40) YA CHUO CHA ARDHI MOROGORO TAREHE 26-11-2021

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Kwa niaba ya Jumuiya nzima ya Chuo cha Ardhi Morogoro na kwa niaba yangu binafsi, ninayo heshima kubwa kukukaribisha wewe Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wageni wengine waalikwa wote katika Mahafali ya Arobaini (40) ya Chuo cha Ardhi Morogoro. Ni dhahiri kuwa, leo hii umeacha majukumu mengine mengi ya kitaifa lakini umeona ni vizuri utuunge mkono kwa kuja kushiriki nasi katika kusherehekea pamoja na vijana wetu wahitimu wa ngazi za Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada katika fani za Upimaji Ardhi pamoja na Mipango Miji kwa mwaka wa masomo 2020/2021.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Ninayo pia heshima kubwa kumkaribisha Mwenyekiti wa Bodi yetu ya Chuo cha Ardhi Morogoro Prof. Sylivester Mpanduji pamoja na wajumbe wote wa Bodi katika Mahafali ya 40 ya Chuo cha Ardhi Morogoro. Hakika pamoja na jukumu kuu la kusimamia Chuo chetu mnayo pia majukumu mengi ya kitaifa lakini leo mmekuja kujumuika nasi katika siku adhimu ya vijana wetu waliohitimu masomo yao.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Kwa namna ya pekee, ninawakaribisha sana kwenye mahafali haya Mhe. Mkuu wa Mkoa wetu wa Morogoro na viongozi wengine wa Serikali ngazi ya Mkoa na Wilaya. Vilevile, ninawakaribisha sana viongozi mbalimbali kutoka Idara na Taasisi za Serikali zilizopo hapa Morogoro zinazoshiriki pamoja nasi leo hii katika mahafali haya.

Shukrani kwa kuja kwenu pia ziwaendee viongozi wa makampuni binafsi, vyombo vya habari, marafiki zetu wa kitaaluma, Chuo cha Ardhi Morogoro, Majirani zetu, Wazazi, Ndugu, Marafiki na wageni wote wa wanafunzi mliokuja kushiriki pamoja nasi katika mahafali haya.

**Asanteni sana na karibuni wote.**

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Chuo cha Ardhi Morogoro ni taasisi ya Elimu inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yako unayoiongoza. Chuo hiki kilianzishwa mahali hapa kilipo, mnamo mwaka 1978 kikiwa tawi la Chuo cha Ardhi – Dar es Salaam, sasa Chuo Kikuu Ardhi (Ardhi University).

Mwanzoni, Chuo hiki kilikuwa kikifundisha kozi ya miezi sita ya mafundi sanifu – upimaji na ramani kwa ngazi ya Astashahada. Hata hivyo, mwaka 1979 mafunzo hayo yalibadilishwa kutoka miezi sita na kuwa ya mwaka mmoja. Mabadiliko zaidi yalifanyika mwaka 1983,

ambapo mafunzo ya fani ya upimaji na ramani kwa ngazi ya Astashahada yalibadilishwa na kuwa ya miaka miwili.

Mafunzo ya Stashahada ya Upimaji yalianzishwa mwaka 2001. Chuo cha Ardhi Morogoro kilipata Ithibati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) mwaka 2009. Kadhalika, Mwaka 2018, Chuo cha Ardhi Morogoro kilianzisha Mtaala mpya wa mafundi sanifu wa fani ya Mipango Miji na Vijiji. Hivyo, Chuo cha Ardhi Morogoro kina fani mbili ambazo ni Jiomatikia pamoja na fani ya Mipango Miji kwa ngazi ya Astashahada ya awali, Astashahada na Shahada.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Chuo cha Ardhi kimeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mpango mkakati wake ambao ulikuwa umejikita katika maeneo yafuatayo:

Maeneo hayo ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi, kuboresha taaluma, kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mitaala ikiwa ni sambamba na kuanzisha kozi mpya, kutoa mafunzo ya muda mfupi, kuendeleza wafanyakazi kitaaluma, kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, kuanzisha kozi mpya ili kuendana na mahitaji ya soko, kufanya tafiti pamoja na kutekeleza miradi mbalimbali ya Kitaalamu.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Naomba uniruhusu kutaja maeneo ambayo tumefanikiwa na yale ambayo tumekutana na changamoto katika kuyatekeleza.

1. **Eneo la Taaluma:**

   - Chuo kimefanikiwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kutoka wanafunzi 49 mwaka 1978 hadi wanafunzi 524 mwaka 2020/2021. Ongezeko hilo linahusisha ongezeko la wanafunzi wa Jinsi ya kike kutoka wanafunzi 2 mwaka 1978 hadi wanafunzi 157 mwaka 2020/2021. Malengo ya Chuo katika udahili ni kufikisha wanafunzi 1,000 mwaka 2023.

   - Chuo kimefanikiwa kuanzisha kozi ya Mipangomiji ambayo ilianzisha mwaka 2018 na mwaka huu tunakamilisha mapitio ya Mitaala ya Jiomatikia na Mipangomiji ili kujitathmini kabla ya kuanzisha kozi nyingine mwaka 2022.

2. **Ushauri wa Kitaalamu**

Chuo cha Ardhi Morogoro kimekuwa kikitekeleza miradi mbalimbali ya Kitaalamu kwa ajili ya kuwajengea watumishi wake uwezo wa kutekeleza majukumu yao ya kufundisha na kufanya tafiti, kuingiza mapato pamoja na kutoa mchango wake kwa Umma kama Taasisi ya Umma.

Katika eneo hili, kwa nyakati tofauti, Chuo cha Ardhi Morogoro kimefanikiwa kufanya miradi mbalimbali katika maeneo yafuatayo, kutaja kwa uchache:

a) Upimaji wa Makao Makuu ya wilaya za Mvomero, Chemba, Kyerwa na Morogoro Vijijini.
b) Upimaji wa viwanja katika majiji ya Arusha, Tanga, Dar es Salaam na Dodoma.
c) Upimaji wa Viwanja katika Halmashauri za manispaa za Iringa, Bukoba, Shinyanga, Moshi, Singida na Morogoro.
d) Upimaji wa Viwanja katika Halmashauri za wilaya katika mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara, Njombe, Geita, Tabora, Songwe na Kigoma.
e) Upimaji wa maeneo mbalimbali ya mashirika na mamlaka za serikali kuu zinazosimamia bandari, hifadhi za taifa, n.k
f) Chuo kimekuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa miradi ya urasimishaji makazi hapa nchini, kwa kushirikiana na halmashauri na wanachi wanaomiliki ardhi katika makazi yaliyoendelezwa kiholela. Miradi hii imetekelezwa katika Mikoa ya Morogoro, Iringa, Arusha, Kilimanjaro pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam
g) Katika utekelezaji wa miradi hii, Chuo kimefanikiwa kupima jumla ya viwanja 30,188 kupitia miradi ya Urasimishaji inayoendelea nchini.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

katika utekelezaji wa mradi hii ya Urasimishaji Makazi pamoja na miradi mingine, naomba kutoa shukrani za pekee kwako wewe binafsi na Wizara yako kwa maelekezo mbalimbali na uwezeshaji wa kifedha ambao kwa kiasi kikubwa ndio umewezesha kukamilisha baadhi ya miradi hii. Naomba upokee taarifa kuwa, kwa kipindi cha mwaka mmoja, tumefanikiwa kukamilisha miradi kwenye Mitaa 17 ambapo jumla ya viwanja 19,930 vimeidhinishwa.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

3. Eneo lingine tunalolishughulikia kama Taasisi ni uendelezwaji wa watumishi.

   Katika Mwaka 2020/2021 Chuo kimesomesha watumishi wake saba, ikiwa watumishi wawili (2) wanasoma shahada ya uzamili na mmoja shahada ya kwanza. watumishi (4) wamesoma kozi fupi tofauti tofauti kulingana na kada zao. Aidha watumishi (32) walipata mafunzo elekezi na upekuzi pamoja na mafunzo ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Aidha, katika eneo la utumishi, Chuo kimefanikiwa kupata kibali na kuajiri watumishi 2 ambao ni wakufunzi wa fani ya Mipango Miji, tumefanikiwa kupata Muundo mpya wa Chuo pamoja na kuwapandisha vyeo watumishi mbalimbali kulingana na mwongozo uliotolewa na Katibu Mkuu utumishi.

**Ndugu Mgeni Rasmi**,

4. Katika eneo la Miundombinu, Chuo kimeendelea na maboresho ya miundombinu ya kufundishia ikiwa ni sambamba na mpango mkakati wa ujenzi wa Chuo katika eneo letu lililopo Mlima Kola.
   - Hapa Chuoni, tumefanikiwa kuanzisha ujenzi wa jengo la darasa ambalo liko katika hatua ya msingi. Jengo hilo litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 215 kwa wakati mmoja na limeunganishwa na huduma za vyoo pamoja na stoo ya kuhifadhia mitihani.
   - Katika eneo la Mlima kola tunakopanga kujenga Chuo, tunaendelea na maandalizi ya mpango kina wa matumizi ya

ardhi (Master plan) na tunatumaini kuwa, fedha tutakayoikusanya kutoka katika miradi inayoendelea itasaidia katika kuanzisha uendelezaji wa eneo hilo.

**Ndugu Mgeni Rasmi**,

Pamoja na mafanikio, ziko changamoto chache ambazo naomba kuziwasilisha kwako na kama kutakuwa na uwezekano, utusaidie kuzitatua.

1. Uendelezaji wa eneo la ekari 33 (hekta 9) lililoko Mlimakola katika Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya kupanua wigo wa mafunzo, miundo mbinu na kuongeza udahili wa wanafunzi. Mpango huu utawezekana tu iwapo Serikali kupitia Wizara yako Mgeni Rasmi itatoa kipaumbele katika ujenzi wa eneo hilo.

2. Madeni ya wazabuni na ufinyu wa bajeti umechangia kuwepo kwa upungufu wa vifaa vya kufundishia hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa Chuo .

3. Pia Chuo kina upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia mfano; tuna seti 3 tu ya GPS, Total station 6 (kati ya hizo tatu ni mbovu). Upungufu huu wa vifaa unaathiri sana mafunzo kwa njia ya vitendo. Tunaishukuru wizara kwa kutupatia vifaa vilivyonunuliwa kwa mkopo wa benki ya dunia. Tunaomba wizara iendelee kutusaidia vifaa kadri vinavyopata.

4. Aidha, chuo kinazo changamoto zingine kama usafiri (Chuo kina gari mbili tu), tunaomba ukisaidie chuo kipate gari jipya.

5. Kuna changamoto ya upungufu wa watumishi katika idara ya taaluma. Juhudi zitafanyika kufuatilia kupitishwa kwa ikama na kupata vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

6. Uchakavu wa miundo mbinu: mfano, majengo na mabomba ya maji, pamoja na Ujenzi wa Maktaba kutokamilika kwa muda mrefu ,na uhaba wa mabweni kwa wanafunzi; ni changamoto zitakazoondolewa endapo chuo kitapata fedha za kutosha kutoka katika miradi ya upimaji ambayo imekamilika.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Katika Mahafali ya arobaini kuna jumla ya wahitimu **376**. Kati yao **112** ni wa kike na **136** ni wa kiume. Wahitimu wa Stashahada ya Jiomatikia (NTA level 6 Ordinary Diploma in Geomatics) ni **101**, wahitimu wa cheti (NTA 5-Technician Certificate in Geomatics) ni **84** na cheti cha awali (NTA 4- Basic Technician Certificate in Geomatics) ni **102**.

Wahitimu wa Stashahada ya Mipango Miji (NTA level 6 Ordinary Diploma in Urban na Regional Planning) ni **26**, wahitimu wa cheti (NTA 5-Technician Certificate in Urban na Regional Planning) ni **29** na cheti cha awali (NTA 4- Basic Technician Certificate in Urban and Regional Planning) ni **34**.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kukushukuru tena kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika mahafali haya. Nawashukuru Wajumbe wa Bodi kwa kusimamia vyema shughuli za Chuo hiki, nawashukuru wageni wote waalikwa na wahitimu. Sina budi pia kuwashukuru wakufunzi wote pamoja na jumuiya nzima ya Chuo cha Ardhi Morogoro kwa mchango wao katika kutoa huduma na kufikia mafanikio makubwa tunayoyasherekea leo hii. Naishukuru kamati ya mahafali ambayo katika kipindi kifupi imefanya kazi kubwa na nzuri.

Mwisho nakuomba Mwenyekiti wa Bodi uchukue fursa hii kutoa hotuba yako na hatimaye umkaribishe Mgeni Rasmi aongee na hadhara hii.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**